MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

1. Taja Sauti Mbili Zinazotamkiwa Kwenye Midomo

2. Taja Irabu zifuatazo

(a) Ya kati inayotamkiwa mdomo ukitandazwa.
(b) Ya nyuma Mdomo ukiviringwa

3. Eleza Maana mbili Zinazojitokeza Katika Sentensi hii
Alimpigia Mpira

4. Tambua aina za Maneno katika Sentensi Ifuatayo

Mwalimu Mrefu anaandika Vizuri sana

5. Unganisha Sentensi Mbili zifuatazo kuunda Sentensi moja moto
Kombe ni dereva mzuri.
Kombe hapendi kuendesha gari

6. Andika kinyume Cha Sentensi zifuatazo
(i) Kuna Watu Wengi Chumbani

(ii) Alipoinama nilifurahi

7. Andika Sentensi zifuatazo katika Wingi
(i) Popo anaruka akitua Mgombani
(ii) Sokwe alikwea mti huu kwa kasi

8. Andika katika Umoja.
Kina mama wale wanafanya biashara

9. Akifisha Sentensi zifuatazo:
mwalimu kazungu alimuuliza mwanafunzi je
unataka kunidanganya ulifika shuleni mapema

10. Eleza Matumizi Mawili ya kila alama ya
kuakifisha ifuatayo
(a) Parandesi
(b) Mstari

11 Tunga Sentensi moja kubainisha tofauti
kati ya maneno haya:
(a) Paka na baka
(b) Suka na shuka.

12a Viyeyusho ni nini?

(b) 12 Andika Sauti zozote mbili ambazo ni
Viyeyusho

13 Nini maana ya kiimbo

Kiswahili

FASIHI SIMULIZI

1. Hini Maana ya fasihi Simulizi

2. Eleza tanzu zozote za Fasihi Simulizi

3a Fafanua Umuhimu wa fomula ya kufungua katika hadithi ( AL 5)

(b) Eleza Umuhimu wa Fomula ya kufunge katika hadithi

4 Eleze Taja na Ueleze Sifa za Mtambaji bora.

LSIMU JAMII

(A) Fafanua maana ya Lugha

(b) Eleza dhima ya Lugha katika Jamii

c. Jadili Kaida Zinazoathiri Mawasiliano